

Orodha Kaguzi ya Uthibitishaji

Tumia picha ambayo mwalimu wako anawasilisha kwa ajili ya zoezi hili ili kujibu maswali yaliyo hapa chini. Tafadhali tathmini kila kitu kwenye Orodha Kaguzi iliyo hapa chini kisha uandike majibu yako kwa kila swali. Fikiria nyenzo za mtandaoni au za nje ya mtandao unazoweza kutumia, nani unayeweza kuongea naye na vidokezi gani kwenye picha vinavyoweza kukusaidia kujibu kila swali.

1 **ASILI:**
Tafuta nakala ya asili ya picha hii na utambulishe wapi uliipata.

2 **CHANZO:**
Tambulisha jina na jina la mtumiaji la mtu aliyepiga picha hii.

3 **TAREHE:**
Tambulisha ni wakati gani picha hiyo ilipigwa. Tafadhali jumuisha mwezi, siku na mwaka.

4 **MAHALI:**
Tambulisha mahali ambapo picha hii ilipigiwa.

5 **NIA:**
Orodhesha kile unachoamini kuwa ni chanzo na nia ya kupiga picha hii na kuisambaza.

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Facebook na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.